**Je, wewe ni kiongozi wa Sayansi ya Mazingira Barani Afrika? Ruzuku ya Utafiti ya Jennifer Ward Oppenheimer (JWO) inakutafuta.**

Katika mandhari pana ya Afrika, ambako maarifa hukutana na uwezo usiotumiwa, watafiti shupavu wanaweza kuwa na athari kubwa huku wakiweka bara hili kwenye ramani ya ubora wa kimataifa.

Ruzuku ya Utafiti ya Jennifer Ward Oppenheimer (JWO) ni ishara ya matumaini kwa sayansi ya mazingira na inaendelea kuwaongoza watafiti vijana ili kuwawezesha kufaulu.

Ikiwa katika mwaka wake wa saba, ruzuku hii inatafuta mpokeaji mwingine mwenye maono makubwa, ambaye kazi yake italeta uwazi, ubunifu, na suluhisho endelevu kwa changamoto kubwa zaidi za mazingira barani Afrika.

Kihistoria, Afrika imekuwa imeachwa nyuma katika nyanja ya utafiti wa kimataifa, huku rasilimali chache zikitolewa kwa wanasayansi wake ikilinganishwa na maeneo mengine. Ilhali, ndani ya mifumo yake anuwai ya ikolojia na jamii madhubuti, kuna uwezo usio na kikomo wa utafiti wa kisayansi wa hali ya juu. Ruzuku ya Utafiti ya JWO inatoa mwanga wa matumaini kwa wanasayansi wa Kiafrika kuwa viongozi wa ubunifu wa mazingira na kuchangia hazina ya maarifa ya dunia.

Ruzuku ya Utafiti ya Jennifer Ward Oppenheimer (JWO Grant) ilianzishwa mwaka wa 2019 ili kuheshimu kazi na sifa za marehemu Jennifer Ward Oppenheimer, mwanzilishi mtajika katika elimu na sayansi ya mazingira barani Afrika. Ruzuku ya Utafiti ya JWO imetoa mchango mkubwa katika kuendeleza mipango muhimu ya utafiti katika bara zima. Inapokaribia mwongo mmoja wa kuwepo kwake, Ruzuku ya JWO inalenga kuvutia idadi kubwa zaidi ya wanasayansi wanaoanza taaluma yao ya kisayansi kutuma maombi ya ufadhili katika mwaka wa 2025, ikiwapa fursa ya kupokea tuzo inayouleta mabadiliko.

Katika kipindi cha miaka sita iliyopita, wasomi wanaoanza taaluma yao na wanasayansi waliobobea katika taaluma mbalimbali za kimazingira kama vile bayoanuwai, plastiki ndogo, na vienezaji vya magonjwa wametafuta ruzuku hii kwa shauku ili kuchunguza mada bunifu za utafiti zinazolenga kushughulikia changamoto za kipekee zinazokabili mazingira asilia ya Afrika.

Dkt. Duncan MacFadyen, Mkuu wa Utafiti na Uhifadhi wa Oppenheimer Generations, alisisitiza mchango mkubwa ambao Ruzuku ya JWO inatoa katika kuendeleza na kukuza maarifa ya Afrika.

MacFadyen alisema "Hii ni tuzo ya kipekee inayoshughulikia pengo muhimu katika maendeleo ya wanasayansi wachanga wa Kiafrika." "Ingawa kila mwaka kuna mshindi mmoja tu, tunawahimiza wale waliowahi kuomba Ruzuku ya JWO kujaribu tena. Tunatarajia kupokea maombi anuwai ya utafiti kwa toleo la saba la Ruzuku ya Utafiti ya JWO. Tuna imani kwamba michango itakayotolewa na watakaoshinda itaendelea sio tu kuboresha jinsi tunavyosimamia mazingira yetu ya asili, bali pia kuhakikisha maendeleo endelevu ya sayansi yenye athari kubwa katika bara letu. Tunaamini kwa dhati kuwa ruzuku hii inawawezesha wanasayansi walio katika hatua za awali za taaluma zao kuendeleza kazi zao na kupendekeza suluhisho mpya na bunifu zinazosaidia kuendeleza Afrika kwa njia endelevu," alisema

Utafiti huu hautoi tu mwanga kuhusu masuala muhimu ya mazingira lakini pia unachangia kikamilifu katika kutoa mitazamo ya Kiafrika katika mijadala ya kimataifa kuhusu uendelevu.

Mshindi wa tuzo ya mwaka uliopita, mwanabiolojia wa mabadiliko ya tabianchi, Dkt. Shannon Conradie, anaboresha uelewa wetu wa nafasi za joto katika kutabiri hatari za joto kwa spishi za wanyamapori kutokana na hali mbalimbali za mabadiliko ya kimataifa katika mifumo ya nchi kavu na maji safi barani Afrika. Pendekezo lake la mradi wa Ruzuku ya Utafiti ya JWO, lenye mada "Kuunganisha

Fizikia na Biolojia ili Kuelekeza Uhifadhi wa Wanyamapori katika Mabadiliko ya Kimataifa", linachukua mtazamo wa taaluma nyingi ili kushughulikia changamoto hizi za dharura. Kwa kuunganisha data kuhusu fiziolojia na tabia katika mifano ya kimitambo, Conradie anafichua jinsi mabadiliko ya mazingira yanavyoathiri usambaaji wa spishi, uhai wao, na matokeo ya kuzaliana.

Utafiti wa Conradie unatumia teknolojia ya kisasa, ikiwemo uchunguzi wa mbali, droni za joto, na uundaji wa mifano ya kibayolojia na kimaumbile, ili kutathmini jinsi spishi zinavyoitikia mabadiliko ya kimataifa katika maeneo makubwa.

Mshindi wa mwaka wa 2023, Dkt. Lovanomenjanahary Marline mwanabrolojia kutoka Madagaska, alitumia ruzuku yake kuchunguza jinsi brolojiana licheni zinavyoweza kutumika katika ufuatiliaji wa hatari kuu za kimazingira na afya ya binadamu kama vile kupotea kwa bayoanuai, mabadiliko ya tabianchi, na uchafuzi wa hewa. Kwa msaada wa Ruzuku ya Utafiti ya JWO, Dkt. Marline alishirikiana na watafiti na wanafunzi kutoka kote barani Afrika kuendeleza utafiti wake.

Athari chanya za Ruzuku ya Utafiti ya JWO zimewafikia wengi tangu ilipoanzishwa.

Tuzo ya kwanza kabisa ilitolewa kwa Dkt. Hayley Clements kwa mradi wake: "Kupima Mipaka ya Bayoanuwai ya Sayari Barani Afrika".

Dkt. Bernard Coetzee, Dkt Gideon Idowu na Dkt. Elizabeth le Roux waliheshimiwa kwa kuwa wapokeaji wa Ruzuku ya Utafiti ya JWO mnamo mwaka 2020, 2021 na 2022, mtawalia.

Utafiti wa Dkt. Le Roux ulilenga kuoanisha michakato ya kiikolojia na uchumaji riziki wa jamii za maeneo husika licha ya kuwepo kwa ongezeko la kutengwa kwa maeneo ya Kiafrika yaliyohifadhiwa.

Dkt. Idowu, kutoka Nigeria, alisisitiza umuhimu wa kuchunguza vichafuzi vya kemikali na plastiki ndogo katika mifumo ya maji safi barani Afrika. Utafiti wake wa kibunifu ulivukaa muktadha wa bahari ambao umechunguzwa vyema, ukichunguza athari za muda mfupi na mrefu kwa afya ya binadamu.

Utafiti wa Dkt. Coetzee ulilenga kuelewa athari za matumizi ya mwanga uliobuniwa na wanadamu kwa bara la Afrika na nafasi yake katika kusambazaa magonjwa yanayoenezwa na wadudu kama vile homa ya dengue, virusi vya Zika na malaria.

Ruzuku ya JWO imebadilika na kuwa chanzo muhimu cha usaidizi kwa watafiti na watu binafsi waliojitolea kukuza Afrika iliyo bora zaidi, kiuchumi na kimazingira. Programu hii haileti tu mabadiliko chanya bali pia inawawezesha wanasayansi wanaoanza taaluma yao kushughulikia majanga ya mabadiliko ya tabianchi ya sasa.

JWO inatoa wito kwa wanasayansi wa Kiafrika wanaoanza taaluma yao kutuma maombi ya ufadhili na kutekeleza utafiti wao wa kiuvumbuzi ili kupata nafasi ya kuleta mabadiliko ya kudumu.

**Mahitaji ya Kupata Ufadhili**

1. Mtuma maombi ya ufadhili anapaswa kuwa mwanasayansi Mwafrika anayeanza taaluma yake na aliye na uhusiano thabiti na taasisi ya Kiafrika inayoaminika na anayependekeza kufanya utafiti katika bara la Afrika.
2. Ruzuku ya Utafiti ya JWO ya 2025 inahimiza maombi ya utafiti yenye mwingiliano taaluma yanayoonyesha uhusiano thabiti kati ya bayoanuwai na uhifadhi.
3. Lazima mtuma maombi ya ufadhili awe na shahada ya Uzamifu (PhD) na asiwe na zaidi ya miaka saba ya kazi na /au uzoefu wa utafiti baada ya kupata shahada yake (isijyoumuisha mapumziko kutoka kazi, pamoja na mapumziko yanayohusiana na majukumu ya kifamilia).
4. Lazima taasisi yake iwe na uwezo uliothibitishwa wa kusimamia ufadhili na iwe inayotumia mbinu bora za usimamizi wa ruzuku ya ufadhili wa kifedha.

5. Uhusiano wa kitaasisi unaweza kuwa wa kitaaluma, kiutafiti, kiserikali, ya Mashirika Yasiyo ya Serikali (NGO), au ya shirika la faida.

**Tuzo ya Ruzuku**

Ruzuku ya JWO ya 2025 ya $150,000 (USD) itatolewa kwa mtuma maombi ya ufadhili mmoja atakayefaulu. Ruzuku hii itasaidia mpango wa utafiti wa hadi miaka mitatu. Kutakuwepo na wito wa maombi mapya ya mapendekezo ya ufadhili kila mwaka (utafiti uliofadhiliwa hapo awali hautastahiki), na mpokeaji ruzuku atatangazwa kwenye Kongamano la Utafiti wa Oppenheimer mnamo tarehe 16 Oktoba 2025.

Ili kutuma maombi ya kupata ruzuku ya ufadhili ya JWO, tafadhali fuata kiungo hiki - https://jworesearchgrant.org/

**Muda wa kutuma maombi ya ufadhili utafunguliwa kuanzia tarehe 24, Machi 2025 na kufungwa tarehe 3 Mei 2025.**

**Kuhusu Utafiti na Uhifadhi wa Oppenheimer Generations**

Timu ya Utafiti na Uhifadhi wa Oppenheimer Ganarations (Oppenheimer Generations Research and Conservation) inaendelea kuunda taasisi ya utafiti ya kiwango cha juu

ambayo inashirikiana na watafiti wa kitaifa na kimataifa

kufanya utafiti wa kisasa unaolenga kuchunguza sayansi asilia inayohakikisha kuwepo kwa matokeo ya kiuhalisia na

yenye athari nzuri. Timu hii imejitolea kuendeleza zaidi, kupanua, na

kukuza ukuaji wa programu na mitandao ya uhifadhi endelevu katika

bara zima la Afrika.

Kwa taarifa za vyombo vya habari, tafadhali wasiliana na:

Yves Vanderhaeghen: yves@jivemedia.co.za

Au

Mihlali Doko: mimi@jivemedia.co.za